**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA**

Namba za Simu
Mkuu wa Shule: 0767594689/0719484090
S.L.P. 11

Shule ya Sekondari ya Ufundi Ifunda,

**IFUNDA.**

**25 May 2021**

Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi

..........................................................
S.L.P. ...............................................
..........................................................

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI IFUNDA HALMASHAURI YA WILAYA IRINGA MKOA IRINGA MWAKA 2020**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2021 tahasusi ya ............................

Shule ya Sekondari ya Ufundi Ifunda ipo umbali wa Kilometa 40 kandokando ya barabara iendayo Mbeya kutoka IRINGA mjini.

Usafiri wa basi kutoka Iringa mjini hadi Ifunda unapatikana katika kituo kikuu cha mabasi na nauli ni shilingi 1,500/= (elfu moja mia tano tu).

Muhula wa masomo unaanza 5Julai 2021, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 02/07/2021. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 0 5 / 07/2021.

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare ya Shule

a) Mashati meupe/blauzi ya mikono mirefu tetron mawili (2) au zaidi.

b) Viatu vyeusi visigino vifupi rangi nyeusi jozi mbili au zaidi.

c) Nguo za michezo Bukta 1( nyekundu kwa wavulana, kwa waschana ya blue), na raba jozi 1 au zaidi uje nazo

d) Soksi rangi nyeupe jozi mbili au zaidi.

e) Taulo na nguo za ndani za kutosha, blanketi 1, mashuka 2 ya kulalia, shuka 1 bluu bahari (light blue) la kutandika juu ya kitanda (bed cover) mto na foronya light blue na chandarua.

f) Pull neck Nyeupe

g) Suruali/Sketi ndefu dark blue mbili na koti la suti dark blue.

h) Track suit nyekundu kwa wavulana na Track suit light blue kwa wasichana.

j) Tai moja rangi ya dark blue yenye nembo ya shule zinapatikana shuleni.

k) T-shirt ya rangi ya Dark Grey yenye nembo ya shule inapatikana shuleni kwa gharama ya Tsh 12,000/=.

l) T-shirt Nyekundu (form six) vazi baada ya masomo isiyo na maandishi yoyote wala picha.

m) Jacket zito jeusi lisilovuka magoti na lisilokuwa na kofia kwa ajili ya kujikinga na baridi wakati wa maandalio ya jioni.

n) Kofia (mzula) wenye rangi ya bendera ya taifa ya Tanzania kwa ajili ya kujikinga na baridi.

**<u>Hijabu kwa wasichana wa kiislamu:</u>**

o. Sketi ndefu mbili (02) (Suruali Hairuhusiwi)

p. Hijabu ndefu zenye kufunika mikono (sio mitandio)

q. Nusu kanzu ndefu na yenye upana wa kutosha.

**ZINGATIA: NGUO ZA NYUMBANI HAZIRUHUSIWI KUJA NAZO.** Mwanafunzi akipatikana nazo atarudishwa nyumbani (kusimamishwa masomo).
**PIA NGUO ZENYE KUSHONWA KIHUNI, ZINAZOBANA, FUPI,NA MAPAMBO YOYOTE KAMA VILE KUPAKA RANGI KUCHA, KUWEKA DAWA NYWELE, KUSUKA NYWELE, KUNYOA PANK, KUNYOA UPARA, HELENI, MIKUFU, PETE N.K. HAVIRUHUSIWI SHULENI.**

**2.2 Ada na Michango ya Shule:**

a) Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi 70,000/=. Unaweza kulipa shilingi 35,000/= kwa nusu muhula au kulipa ada yote kwa mara moja. Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule Na. 60501100041 katika Benki ya NMB. Jina la akaunti ni Ifunda Technical Secondary School. (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip na mchepuo wake).

**b) Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni:-**

i. Shilingi 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani

ii. Shilingi 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha

iii. Shilingi 20,000/= kwa ajili ya taaluma

iv. Shilingi 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine

v. Shilingi 2,000/= nembo ya shule

vi. Shilingi 10,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza Tshs. 5,000/= na Bima ya Afya Tshs. 5,000/=

vii. Shilingi 20,000/= mitihani ya kujipima mock Mkoa kwa kidato cha Tano.

viii. Fedha ya tahadhari 5,000/= (haitarejeshwa)

Fedha zote za michango ziwekwe kwenye akaunti ya shule Na. 60501100041 NMB Benki. Jina la akaunti ni Ifunda Technical Secondary School.

**Angalizo:** Jumla ya ada na michango kwa wanafunzi wa:-

(i) Bweni ni shilingi 188,000/=

**(ii) Mwanafunzi anapokuja anatakiwa kulipa kiasi cha**

**TSH.** 153,000/= kwa muhula wa kwanza

**c) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-**

(i) Godoro la sponji inchi 3 x 6 unaweza kununua kwenye maduka karibu na Shule kwa bei ya TSH 70,000/=.

(ii) Chombo kwa ajili ya chakula, kikombe 1 na kijiko 1

(iii) Ream 2 za karatasi (Photocopy A4) utaikabidhi kwa Mwl. Msajili.

(iv) Vitabu vya masomo, kila mwanafunzi aje navyo kulingana na tahasusi aliyochaguliwa.

(v) Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biolojia

(vii) Scientific calculator kwa wanafunzi wanaosoma michepuo ya (PCM,PCB,PGM na CBG).

**VIFAAA VYA KUFANYIA USAFI VYA KUJA NAVYO MWANAFUNZI WA KIDATO CHA TANO.**

**PCM: Mkasi mmoja wa maua, Ndoo kubwa moja na chelewa.**

**PCB: Jembe, Kwanja, Squizer, soft bloom, Hard bloom Ndoo ndogo mbili na chelewa.**

**CBG: Jembe, kwanja, Squizer, soft bloom, Hard bloom Ndoo kubwa moja na chelewa**

**PGM: Panga, kwanja, Squizer, Soft bloom, Hard bloom, Ndoo ndogo mbili na chelewa.**

**HKL: Reki, kwanja, squizer, Ndoo kubwa na chelewa**

**HGL: Jembe, Kwanja, Squizer, Soft bloom, Hard bloom, na chelewa.**

**HGK: Mopa na ndoo yake,Spedi, Squizer, soft bloom, Hard bloom.**

**3. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE:**

(i) Wizi

(ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro

(iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo

(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla

(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote yule (vi) Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzo wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususiuliokubalika na uongozi wa shule.

(vii) Kufuga ndevu

(viii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.

(ix) Uvutaji wa sigara

(x) Uasherati,Kujihusisha na Mapenzi shuleni, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa

(xi) Kupata ujauzito au kutoa mimba

(xii) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunjua sheria za nchi.

(xiii) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.

(xiv) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni

(xv) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi au vifaa vyake (phone accessories) katika mazingira ya shule.

(xvi) Kudharau Bendera ya Taifa.

(xvii) Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.

(xviii) Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

4. **Viambatisho na Fomu Muhimu:**
    a) Fomu ya uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali.
    b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makossa ya jinai.
    c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
    d) Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule: .....................................**

**Jina la Mkuu wa Shule: .........................................**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule: ...................................**

**Nakala:-**

1. Katibu Mkuu,
   Ofisi ya Rais,
   TAMISEMI,
   S.L.P. 1923,
   **DODOMA.**

2. Mkurugenzi wa Elimu ya Sekondari,
   Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
   S.L.P. 9121,
   **DAR ES SALAAM**.

3. Mkurugenzi Mtendaji,
   Halmashauri ya Wilaya ya Iringa,
   S.L.P. 108,
   **IRINGA.**

4. Afisa Elimu (M),
   S.L.P. 858,
   **IRINGA.**

5. Afisa Elimu Sekondari (W),
   S.L.P. 642,
   **IRINGA**.

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA**

**SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI IFUNDA**

**<u>Sehemu Mwanafunzi:</u>**

Mimi. …………………………………….................... Msichana/Mvulana ninakubali nafasi niliyopewa kuingia kidato cha ……………................... mwaka …….............. katika Shule ya Sekondari ya Ufundi Ifunda, na nitafika shuleni bila kuchelewa. Nitatii na kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zote za shule na za Nchi.

Nitakuwa Mwanafunzi mwenye bidii katika katika masomo na kazi za Elimu ya Kujitegemea.

**<u>Sehemu ya Mzazi/Mlezi</u>**

Mimi. ……………………………….Ninakubali mtoto wangu kuingia Shule ya Sekondari ya Ufundi Ifunda kidato cha ………………… mwaka ………na

Ninaahidi kumlipia karo ya Shule na kumpatia mahitaji yote kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na Shule (Joining Instructions) ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na Shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa Shule na Taifa.

Anwani yangu ya kudumu ni:

……………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………

Namba ya simu ya mkononi ……………………… ya mezani/ofisini…………….

Iwapo nitapata uhamisho au kubadilisha makazi ni lazima nitaijulisha shule kwa maandishi yaliyothibitishwa na Mkuu wangu wa Idara au Ofisi ya Afisa Mtendaji wa Kata/Kijiji.

Sahihi ……………………………………… Tarehe ………………………….

**JAZA FOMU HII NA KUIRUDISHA SHULENI WAKATI WA KURIPOTI.**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA**

**SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI IFUNDA**

**S.L.P. 11,**

**IFUNDA**

**TAARIFA YA BINAFSI YA MWANAFUNZI**

1. Jina ……………………………………….......................... tarehe ya kuzaliwa (tarehe,mwaka na mwezi)…………..................., Mkoa aliko zaliwa ……..…………………………………………..
2. Kabila …………………………………………………………. Taifa ………………………….…......
3. Dini na madhehebu ………………………………………………………….……………..........
4. Jina la Baba …………………………………………………………………………........................
5. Anwani ya Baba ……………………………………………………………………….....................
   ………………………………………………………………………………………………………………….
6. Kazi ya Baba ………………………………………………………………………….......................
7. Jina la Mama ……………………………………................... Kazi yake ……………...............
8. Wazazi wanaishi pamoja au wametengana……………………………………….............
9. Jina na anwani ya Mlezi wako (kama si Mzazi) ………………………………...............
   ………………………………………………………………………………………………………………….
   ………………………………………………………………………………………………………………….
10. Wakati wa likizo utakwenda kwa nani na wapi ……………………………...............
    (taja sehemu moja tu utakakokwenda kila wakati)..........................................
    ………...........................................................................................................
11. Hapa Mkoani Iringa nina/sina ndugu…………………………………………….............
    Endapo una ndugu jaza jedwali lifuatalo hapa chini.

| JINA LAKE | UHUSIANO | MAHALI ANAPOISHI | ANWANI NA NAMBA YA SIMU |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

12 Ninathibitisha kwamba habari zote nilizotoa ni kweli na sahihi
   Sahihi ya Mwanafunzi…………………………………………….. Tarehe: …………….........
   Sahihi ya Mzazi/Mlezi ……………………………………………. Tarehe ……………….......
13. Jina na sahihi ya Afisa Mtendaji wa Kijiji ……………........................................
    Mhuri: ...................................................................

**PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENTS**
**IRINGA DISTRICT COUNCIL**

**IFUNDA TECHNICAL SECONDARY SCHOOL**

## FORM MEDICAL EXAMINATION

(To be completed by a Medial Officer in respect of all Form I entrants)

Pupil's full name……………………………………………………………………………………………

Age …………………………………………….......      years Sex ………………………

Blood count (Red and white) …………………………………………………………………………

Stool Examination …………………………………………………………………………………………

Syphilis and other venereal diseases test ……………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

T.B. Test …………………………………………………………………………………………………………

Eye Test …………………………………………………………………………………………………………

Ears ………………………………………………………………………………………………………………

Spleen ……………………………………………………………………………………………………………

Abdomen …………………………………………………………………………………………………………

Urine for plamotest ………………………………………………………………………………………

Test for pregnancy (for girls only) ………………………………………………………………

**ADDITIONAL INFORMATION**

(If any) e.g. physical defects, impartments e.g legrete)

Infections, chronic of family diseases etc ……………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………

**I certify that the above is fit to pursue studies in Technical Education.**

Station……………………… Signature …………………………………………

Date ……………………….. Designation ……………………

**OORODHA YA VITABU AMBAVYO MWANAFUNZI ANATAKIWA KUJANAVYO KULINGANA NA MCHEPUO WAKE AU TAHASUSI YAKE**

## PURE MATHEMATICS;

1. Pure mathematics I and II by J, K Backhouse.
2. Advanced level pure mathematics by Kinunda.
3. Advanced level pure mathematics by C.J Tranter- 2006
4. S.Chand mathematics for class XI, volume I and II by H.K DASS R.VERMA 2013
5. Calculator Casio.

## BASIC APPLIED MATHEMATICS (BAM):

1. Basic applied mathematics for Advanced school form V and VI by Septine .I

## BIOLOGY:

1. Fundermental of biology (2018) by Godfrey mwaniki.
2. Biology class X1 by Dr P.SVerne,Dr B.P PANDEY,CHAND
3. A text book of CBSE Biology for class XI by Sarital Aggrarwal

## CHEMISTRY:

1. Conceptual chemistry for class XI by S.Chand
2. Conceptual chemistry for class XII BY S. Chand
3. Chemistry for Alevel Third and forth edditin by Ted Listers and Janeth Renshaw
4. University of illnos Chemistry, Third edition by Stephen S Zumdal
5. Organic chemistry part B by mzumbe book project
6. Advanced Chemistry ,physical and industry chemistry by Philip Mathew Cambridge 2003
7. Chemistry in context,sixth edition by Graham Hill, John Holman Nelson Thornes

## VITABU VYA HISTORY:

1. How Europe underdeveloped Africa by Walter Rodney.
2. Africa since 1800, $4^{th}$ edition by Roland Olive and Atmore.
3. The political economy, imperialism by Nabudere.
4. Mastering Advanced level History book II by Kato.
5. World History Advanced Level by Samweli Mhajida.
6. Focus on modern world History History Advanced Level by Chakupewa.J etal (2012) paper I na Paper II.
7. Contemporary history events volume one first edition by Shibitali C.K
8. Major Events in th. World History paper 2 Advanced Level Gervas.M Zombwe.
9. Pia kitabu chochote cha history kidato cha tano na cha sita.
10. Essential in History paper 11 Written by Yasin

## VITABU VYA GEOGRAPHY;

1. Bunnett (2006) physical geography in diagram for Africa Longman Limited china.
2. Economic geography by Mogarn.
3. Human and economic geography by D.T Msabila.
4. The essential of practical geography Advanced level by Joseph William Njiku (2005).
5. Certificate of Human and economic Geography. By Morgan and Leong Chang.

## VITABU VYA KISWAHILI

**A. USHAIRI:**

1. Kimbunga - G.Gora (Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili) 1999.
2. chungu Tamu-T.A Mvungu (Tanzania published house) 1985.
3. Mapenzi bora-S.Robert (Mkuki na Nyota) 2003.
4. Fungate ya Uhuru M.S Khatibu.

**B. RIWAYA;**

1. Vuta n'Kuvute- A.Shafi (Mkuki na Nyota)-1999.
2. Kufikirika S.Robert-2003
3. Mfadhili –Hussein Tuwa.
4. Usiku utakapokwisha-Mbunda Msokile-2007

**C. TAMTHILIA;**

1. Moran -E.Mbogo
2. Kivuli Kinaishi –Said Mohamed-2007.
3. Kwenye Ukingo wa Thim-E.Ussein
4. Nguzo Mama-1982.

## ENGLISH LANGUAGE;

**A-**

1. New advanced level English by Charles. E
2. Advanced level English, A practical approach by Nicholous Asheli.
3. Advanced level literature by Nyambari Nyangwine.
4. Advanced level Learners Dictionary.
5. Teaching English as a foreign language by G.Broughton.
6. English form V and VII by M. Kadege.
7. Contempory English for advanced level by Francis Mnyawe.
8. Complete course by M.Kadege.

**B-NOVEL:**

1. The beautiful ones are not yet born by A.K Amah.
2. A man of the people by C.Achebe.
3. Divine providence –Mkuki na Nyota.
4. Encounters from Africa –Macmillan.
5. The rape of the peal-Macmillan.

C**-PLAYS/DRAMA;**

1. An Enemy of the people –H.Ibsen.
2. I Will Marry When I want-EAEP
3. Rwanda Magere by Okoti Omtatah-1991
4. The Pride –EAEP
5. Black Mamba-EAEP.

C**-POETRY;**

1. Selected poem from institute of education.
2. The wonderful Surgeon and other poem-Mkuki na Nyota.

## GENERAL STUDIES:

1. Understanding General Studies for a level by Johanes Big Wamungu 2015.